

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA SABA

KIKAO CHA AROBAINI NA SABA

20 JUNI, 2022



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA SABA

KIKAO CHA AROBAINI NA SABA– TAREHE 20 JUNI, 2022

I. DUA:

II. MASWALI:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

411. **MHESHIMIWA JOSEPH KIZITO MHAGAMA (MADABA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itatenga fedha kwa ajili ya kutengeneza Barabara ya Wino hadi Ifinga ambayo wakati wa masika haipitiki.

412. **MHESHIMIWA VINCENT PAUL MBOGO (NKASI KUSINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itajenga Soko katika Mji Mdogo wa Chala Wilayani Nkasi.

WIZARA YA MAJI:

**413. MHESHIMIWA SOPHIA HEBRON
MWAKAGENDA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, ni lini Serikali itaharakisha na kumaliza upembuzi yakinifu kwa ajili ya mradi wa maji katika Vijiji 46 Wilayani Rungwe.

WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:

**414. MHESHIMIWA ABDUL-HAFAR IDRISSA
JUMA (MTONI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:-

Je, ni lini Majimbo ya Zanzibar yatapata fedha za Mfuko wa Jimbo kwa wakati.

**415. MHESHIMIWA ANGELINA ADAM
MALEMBEKA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha stakabadhi za mashine za EFD ili zisifutike baada ya muda mfupi.

WIZARA YA KILIMO:

**416. MHESHIMIWA DKT. DAVID MATHAYO
DAVID (SAME MAGHARIBI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, ni lini Serikali itasaidia kukarabati mifereji ya Marwa, Kwasita, Magereza, Gunge na Kirua katika Bonde la Mto Pangani.

**417. MHESHIMIWA YUSTINA ARCADIUS RAHHI
(VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kukamilisha uwekaji wa samani na vifaa vya kufundishia katika vituo vya rasilimali za kilimo.

WIZARA YA MADINI:

418. MHESHIMIWA ALLY ANYIGULILE JUMBE MLAGHILA (KYELA):


Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Madini:-

Je, uchimbaji wa madini kando ya Mito na Maziwa ni chanzo cha upungufu wa samaki.

III. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:

Kwamba, Bunge sasa likubali Kujadili Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2021 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.



Kwamba, Bunge sasa likubali Kupokea na Kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

(Majadiliano yanaendelea)

**DODOMA
20 JUNI, 2022**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc*
KATIBU WA BUNGE**